



HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA

S.L. P 83, KALIUA, Simu Na: 0736 204 192,
Nukushi: 0732 988 451, Barua pepe: ded@kaliuadc.go.tz,
Tovuti: www.kaliuadc.go.tz

KDC/M.2/VOL.II/0056/38

29/03/2018

TANGAZO LA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua kwa kuzingatia kibali cha ajira Mbadala chenye Kumb Na. CFC 26/ 205/01 "FF"/91 cha tarehe 22 Agosti, 2017 kikisomwa pamoja na barua ya nyongeza ya muda wa utekelezaji wa kibali cha ajira mbadala kwa watendaji wa vijiji / mitaa yenye Kumb. Na. CFC.26/205/"1"GG/95 ya tarehe 12 March, 2018 kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora anawatangazia Watanzania wote wenye sifa nafasi za kazi kama ifuatavyo;-

A. MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III (NAFASI 3)

1. Sifa za Mwombaji

Awe na Elimu ya Kidato cha nne (Form four) au Sita (Form Six) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti (NTA LEVEL 5) katika moja ya fani Zifuatazo;-Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo Dodoma au chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

2. Kazi za kufanya

- i. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya kijiji
- ii. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa amani na msimamizi wa Utawala Bora katika kijiji
- iii. Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kijiji
- iv. Katibu wa mikutano na kamati zote za Halmashauri ya kijiji
- v. Kutafsiri na kusimamia Sera, sheria na Taratibu

- vi. Kuandaa wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishajimali
- vii. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya kitaalamu katika Kijiji
- viii. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za kijiji
- ix. Mwenyekiti wa kikao cha wataalamu waliopo katika kijiji
- x. Kupokea, kusikiliza na kutatua migogoro ya wananchi
- xi. Kusimamia utungaji wa sheria ndogo za kijiji
- xii. Kusimamia ukusanyaji wa mapato katika kijiji
- xiii. Kuandaa na kutunza rejista ya Wakazi wote wa kijiji
- xiv. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata

3. Ngazi ya Mshahara ni kulingana na Viwango vya Serikali TGSB

4. MASHARTI YA JUMLA

1. Mwombaji awe raia wa Tanzania
2. Mwombaji awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45
3. Mwombaji awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela.
4. Maombi yote yaambatanishwe na wasifu wa mwombaji unaojitosheleza (Detailed cv).
5. Maombi yote yaambatanishwe na nakala za vyeti vya taaluma, vyeti vya elimu (IV au VI), cheti cha kuzaliwa na picha moja ya rangi ya hivi karibuni (passport size) iliyoandikwa jina nyuma.
6. "Testimonials", "Provisional results", hati za matokeo ya kidato cha nne na sita (Result slips) "Leaving Certificate" HAVITAKUBALIWA.
7. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vya Taaluma vihakikiwe na TCU na Baraza la Mitihani la Tanzania.
8. Waombaji waliowahi kuacha kazi, kuachishwa au kufukuzwa kazi hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kwa kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.

5. Maombi yatumwe kwa:-

MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA,
S.L.P.83,
KALIUA.

Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ni tarehe 11/04/2018 saa
9.30 mchana.



Dkt. John M. Pima

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
KALIUA**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
KALIUA

Nakala;

Mbao za matangazo

Tovuti ya Halmashauri - www.kaliuadc.go.tz